

# Aflasafe TZ01

## PRODUCT INFORMATION

**Aflasafe TZ01** ni kiwatilifu cha kibaiolojia kwa ajili ya kutumika kwenye mashamba ya mahindi na karanga ili kuwabadili fangasi familia ya *Aspergillus* wanaozalisha sumukuvu. **Aflasafe TZ01** ina fangasi hai waliopakwa kwenye punje ya mtama uliokaangwa unaoutumika kama kibebeo na chakula. Gundi inasaidia fangasi kunatia kwenye punje bila kuachia au kubaki kwenye mikono ya mtumiaji. Rangi ya bluu isiyo na madhara imepakwa kwenye punje ili kutofautisha na punje zinazoliwa na ndege. Baada ya kutawanywa na mara tu punje kupata unyevu wa kutosha, fangasi waliopo kwenye **Aflasafe TZ01** wanaota na kuzaliana. Fangasi hawa wanaoota mwanzoni wanaonekana kama nyuzi nyeupe zikiwa na mbegu za kijani na mwisho wanaonekana kama nyuzi za kijani zikiwa na mbegu. Baadaye mbegu zitasambaa kwenye mmea kwa kupeperushwa na upepo au wadudu kama ambavyo fangasi wanaozalisha sumukuvu wanyosambazwa.

## MAELEKEZO YA JINSI YA KUITUMIA

- Fuata kanuni za kilimo bora kwenye eneo lako la kupanda mazao.
- Kabla ya kutawanya **Aflasafe TZ01**, shamba linatakiwa liwe limepaliliwa, limewekwa mbolea na shughuli nyingine zinazofanyika kwenye kilimo ili kuzuia kukandamizwa kwa punje za **Aflasafe TZ01** baada ya kutawanywa.
- USIFANYE SHUGHULI YOYOTE ITAKAYOFUKIA **Aflasafe TZ01** KWENYE UDONGO BAADA YA KUTAWANYWA. Hakikisha **Aflasafe TZ01** inabaki juu ya udongo.
- Kwa vyote mahindi na karanga tawanya **Aflasafe TZ01** kwa mkono wiki 2 – 3 kabla ya mazao kutoa maua/mbelewele katika kiasi cha kilo 10 kwa hekta.
- Ikiwezekana, tawanya **Aflasafe TZ01** baada ya mvua kunyesha au mvua ikitabiliwa au udongo ukiwa mbichi. Pakiwa na unyevu wa kutosha katika udongo, fangasi wasiozalisha sumu huota haraka kwenye punje iliyobeba ambayo pia ndio chakula chake.
- Siku ya tano hadi saba baada ya kutawanya **Aflasafe TZ01** tembelea shamba lako tazama rangi ya punje iliyotawanyana. Maoteo ya rangi ya kijani kwenye baadhi au punje zote endapo unyevu ni wa kutosha kwenye udongo. Kama uoteo wa kijani sio wa kutosha, tembelea baada ya siku 2 hadi 5 ili kuangalia maoteo ya rangi ya kijani tena.
- Fuata kanuni bora za kuvuna na za baada ya kuvuna.

## TAHADHALI WAKATI WA KUTUMIA

Usitumie pamoja na mbolea au viwatilifu vya kuua vidubini. Tumia **Aflasafe TZ01** iwapo uwezekano wa kuihamishia kwenye maeneo muhimu kama makazi ya watu, maji na sehemu tengefu ni mdogo.

## UHIFADHI NA UTUPAJI WAKE

**Aflasafe TZ01** ISICHAFUE MAJI, CHAKULA KWA KUHIFADHI NA KUTUPA

**UHIFADHI wa Aflasafe TZ01:** Hifadhi ikiwa kavu. Usiiweke kwenye unyevu zaidi ya kiasi cha 80% kabla ya kuitumia. Bidhaa hii ina vidubini vifanyavyokazi vikiwa hai. Usihifadhi kwenye joto lililozaidi ya 50 °C.

**UTUPAJI wa Aflasafe TZ01:** Tumia bidhaa yote kwenye kifungashio kwa kutawanya kwa kufuata maelekezo. Bidhaa iliyobaki itupe kwa kushirikiana na watupaji rasmi wanaotambulika kama vile utupaji unaofanywa na Mikoa, Serikali za Mitaa au na viwanda.

**UTUMIAJI WA VIFUNGASHIO:** Usitumie kifungashio zaidi ya mara moja. Ikiwezekana peleka kifungashio kitupu kwa wachakataji wa vifungashio au tupa kifungashio kwenye shimo la taka au kichomwe moto na Serikali za Mitaa na wakati ikichomwa kaa mbali na moshi.

## MADHARA YA KIMAZINGIRA

Usitumie kwenye maji moja kwa moja au kwenye maeneo yenye maji. Usichafue maji wakati wa utupaji wa vifaa au maji yaliyotumika kuoshea.

Kwa maelezo zaidi, tafadhali wasiliana na:  
IITA-Tanzania, Kitovu cha Afrika ya Mashariki  
Plot No. 25, Eneo la Viwanda Mikocheni  
Mwenge – Barabara ya Coca Cola, Mikocheni B  
P.O. Box 34441, Dar es Salaam, Tanzania  
Simu: +255 22 2700092; USA Simu: +1 201 6336094  
Barua pepe: [iita@cqiar.org](mailto:iita@cqiar.org)